SHULE YA UPILI YA GATITU S.L.P.327,GATUNDU

TATHMINI LA JUNI, KIDATO CHA KWANZA 2015

JINA .....DARASA.....NAMBA:.....

Jibu maswali yote

A.Ufahamu

Baridi ya mzizimo iliyokuwako ilianza kutoweka polepole na kupisha ucheachea wa jua la asubuhi. Moyo wake Rashid sasa ulijawa matumaini mapya. aligusa mtima wa abu yake ambaye alilala kwenye kidibwi cha ngeu huku akivuja damu mithili ya paa livujalo msimu wa masika. Wajihi wake ulidhihirisha dhahiri shahiri kuwa alikuwa mguu mmoja duniani na mwingine kaburini. Hata hivyo Rashid alipiga mtima konde licha ya kuwa machozi yalimlengalenga. Alielewa bayana kuwa ushikwapo shikamana.

Alitupa ozi huko na kule mithili ya wibari nyikani. Licha ya kuwa uchechea wa jua ulikaribisha mwangaza angavu, hangeweza kuona mbali kwani alikuwa porini kwenye miti mirefu na iliyopandwa sako kwa bako. Alijaribu kuinua shingo ima fa ima lakini wapi ! Aliwaona nyani tu waliokuwa wakidandia miti huku wakiduwaa wageni waliojikaribisha kwenye maskani yao walitoka wapi na walitaka nini.Aliwaangalia bila kunena lolote kwani kipofu kumwashia taa ni kuharibu mafuta.

Maskini mtoto wa watu alichanganyikiwa mithili ya mwehu kwani hakujua alikokuwa na jinsi ambavyo angepata auni. **Taswira** iliyotawala akilini mwake ilikuwa jinsi walivyotekwa nyara na kuletwa kwenye msitu huo baada ya kunyang'anywa gari, pesa na chochote cha thamani walichokuwa nacho hata mavazi. Kilichomkera na kunikereketa ni jinsi ***hayawani*** wale walimmiminia abu yake risasi licha ya kuwa hakuthubutu kamwe kukaidi amri yao. Ama kwa kweli, ibilisi wa mtu ni mtu chambilecho wahenga.

Baada ya kuzama kwenye lindi la mawazo, aliamua kujitwika magogo mazito liwalo liwe! Alikata shauri kufuata kijia kimoja akiwa na wingi wa matumaini kuwa angepata msaada alioutafuta kwa udi na uvumba. Alitembea kikakakaka mithili ya askari aliyesikia mbio ya mgambo huku akiwa roho mikononi. Baada ya kutembea kwa muda alisikia sauti za adinasi kwa mbali lakini hangetambua zilikokuwa zikitoka kwa sababu ya mwangwi. Hata hivyo alijikaza kiume kwani aliamini na kusadiki kuwa penye nia pana njia.

1. Pendekeza kichwa/anwani mwafaka ya kifungu hiki. (alama1)

.....

Powered By: www.manyamfranchise.com

2. Ni kwa nini moyo wake Rashid ulijawa na matumaini mapya (alama 2)

.....

.....

1. Licha ya kuwa na mseto wa mawazo na hisia Rashid alionyesha ukakamavu. Dhibitisha .
((alama 2)

.....

.....

.....

2. Mbona Rashid hakuwaelezea wenyeji wake jakamoyo lilomkabili? (alama 1)

.....

.....

3. Elezea maana ya methali hizi kama zilivyotumika katika kifungu (alama4)

(a) Kipofu kumwashia taa ni kuharibu mafuta

.....

.....

(b) Ibilisi wa mtu ni mtu

.....

.....

4. Semi "Kujitwika magogo mazito" ina maana gani jinsi mwandishi alivyoitumia katika kifungu hiki

(alama1)

.....

.....

5. Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika kifungu (alama4)

i)hayawani.....

ii)taswira.....

Powered By: www.manyamfranchise.com

B.*Matumizi ya lugha*

1 kamilisha jedwali. (alama3)

sauti	aina	Mahali pa kutamkia	Ghuna au sighuna
b			
th			

2. Onyesha mahali pa kuwekwa shadda katika maneno yafuatayo. (alama2)

i) mtu.....

ii) mwanafunzi.....

3. Bainisha maneno katika sentensi ifuatayo : (alama 3)

Alienda shuleni lakini hakusoma kitabu chake

.....

.....

4.Badilisha sentensi zifuatazo kulingana na maagizo katika mambano. (alama 2)

i)Mama yake alimchuna sikio (mazoea)

.....

ii) Amu yangu atawalisha ng'ombe (hali ya 'me')

.....

5.Tumia alama zifuatazo za kuakifisha katika sentensi kwa usahihi. (alama2)

i)nukta pacha .....

ii)paradesi :.....

6. huku ukitoa mifano, onyesha njia nne za kuunda silabi za Kiswahili (alama2)

.....

.....

.....

.....

Ukurasa 3

Powered By: www.manyamfranchise.com

7.Toa sifa mbili kwa kila irabu uliyopewa. Alama2)

i) o.....

ii) i .....

iii) e.....

8.Yakinisha katika nyakati ulizotajiwa katika mabano (alama2)

a) Hamkusoma vitabu vya Mzetuni (uliopo)

.....

b) sijamuona akilima (ujao)

.....

9. .majina yafuatayo yamo katika ngeli gani? (alama 2)

Ureno.....

Ujinga.....

bawabu.....

Wadhifa.....

10. .Andika sentensi hii katika hali ya udogo. (alama 2)

Mwizi huyu atasalitiwa na mtoto wake.

.....

11. Tunga sentensi kuonyesha tofauti za kimaana kati ya vitate hivi. (alama 2)

Rithi:..... .....

Ridhi:.....

12Tunga sentensi kulingana na dhana uliopewa: (alama 5)

Sentensi ya taarifa: .....

Powered By: www.manyamfranchise.com

.....

.....

18. Akifisha sentensi zifuatazo: (Alama 3)

a) je utakuja kwetu sikuja ya jumapili

.....

b) kumbuka maneno haya amani umoja na upendo

.....

C.Fasihi

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali

1. Tunda la elimu zote, wanasema wanazuoni
   Ni kwamba mtu apate, kumtambua manani
   Ndipo hadhi apate, akumbukwe duniani.

2. Elimu bila ukweli, haizidi asilani
   Giza na nuru muhali, katu havitangamani
   Uwongo ufe kweli, itue nuru moyoni

3. Elimu ni kama mali, haichoshi kutamani
   Ni bora yashinda mali, taji la wanazuoni
   Elimu njoma miali,langazayo gizani.

4. Mtu hachomwi na mwiba, na viatu miguuni
   Ulimwengu una miiba, tele tele majiani
   Elimu ukiishiba, u salama duniani.

5. Wafu ni wasiosoma, watazikwa ardhini
   Hai ndio maulana,wapaao maangani
   Elimu jambo adhima, aso nayo maskini.

6. Toa wakfu ujana, elimu ukitamani
   Na uwe mzee sana, kujua usijihini
   Elimu ni jambo adhima, aso nayo maskini

Powered By: www.manyamfranchise.com

7. Elimu ina malipo, utoyalipwa mwishoni
   Pale uitafutapo, ujira usitamani
   Mwanachuoni afapo, mbingu huwa na huzuni.

8. Haki ya kuheshimiwa, ni yao wanachuoni
   Wao wameongolewa, na ni taa duniani
   Kweli wanapoijua, watoe bila kuhuni.

9. Elimu bila amali, mti usio majani
   Haumtii kivuli, aukaliaye chini
   Inakuwa mashkeli, wa kughuri insane.

Maswali

a) Toa kichwa mwafaka kwa shairi hili (alama 2)

.....

b) Shairi hili ni la aina gani?Eleza jibu lako. (Alama 3)

.....

.....

c)Eleza umbo la shairi (alama 4)

.....

.....

.....

.....

d)Eleza mshairi anazungumzia nini katika ubeti wa tatu na wa saba ? (alama 6)

.....

.....

.....

.....

Eleza dhima (umuhimu) tatu za fasihi simulizi. (Alama 3)

.....

.....

.....

Powered By: www.manyamfranchise.com

3)Eleza maana ya: (Alama 2)

i.Hekaya:.....

.....

ii.Semi:.....

.....

D: *Isimu-jamii*

1.Fafanua maana ya: (Alama 3)

a) Isimu-jamii.

.....

b) Sajili.

.....

2.Taja mambo yoyote ***manne*** yanayoathiri matumizi ya lugha. (Alama 4)

.....

.....

.....

.....

3.Fafanua sifa zozote ***tatu*** za lugha ya sokoni. (Alama 3)

.....

.....

.....

**********HERI NJEMA**********

Powered By: www.manyamfranchise.com